MITIHANI YA KISWAHILI

SEHEMU YA KWANZA: INSHA (ALAMA 20)

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:
   a. Anza insha yako kwa maneno yafuatayo: Tuliamka asubuhi na mapema kunadhifisha kila mahali kujitayarishia maandalizi ya…….....
   b. Manufaa ya kiswahili kufanywa lugha rasmi nchini Kenya
   c. Andika mazungumzo kati ya mwalimu anayesimamia ushauri Nasaha na mwanafunzi aliyeathiriwa na dawa za kulevya:
   d. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake.

SEHEMU YA PILI: UFAHAMU

2. Soma habari hii kisha ujibu maswali

Ingawa adhabu ya kiboko kwa wanafunzi imepingwa marufuku baada ya shirikizo mbalimbali kutoka sekta tofauti yakiwemo mashirika ya kimataifa kama vile UN, baadhi ya wanamapokeo wameng'ang'ana kwa jino na ukucha kupinga hatua hii.

Madai yao ni kuwa kuondolewa kwa adhabu ya kiboko kungesababisha baadhi ya wanagenzi kulaza damu kwa vile wangewashwa vibiriti wangeweza kusisimuka na kutupilia mbali utepetevu ambao ungewaingia katika harakati zao za kuandama elimu. Kwamba iwapo wao walipigwa kwa nchi hawa wengine wanadai ru kutokana wasipigwe. Wengine wanadai ni kutokana na kutandikwa kwao shuleni ndipo waliweza kutia biddi masomoni wakahitimu kwa viwango vya juu na kuwawezesha kuyapata madaraka wanayoyashikilia serikalini hivi leo.

Kundi hili linazidi kuvutia ngozi upande wao kwa kusema kwamba wanafunzi wasiochapwa aghalabu hudhoofika kinidhamu ambapo wanapeuza baadhi ya kaida

zilizowekwa na kuvimba vichwa kwa wakubwa wao na kufanya kazi kutotekelezwa kwa urahisi. Hivyo basi wanaonelea adhabu hii ni muhimu kwa minajili inakuwa kama mwongozo wa wanafunzi kufuatataratibu za shule kila siku hadi juma zima, muhula mzima hadi mwaka nzima. Bila kucharazwa, kwao inaonekana kuwa wanafunzi hawatafika shuleni mapema inavyotarajiwa, vilevile hawataingia darasani mapema, kushiriki shughuli zote za shule vizuri hata kuheshimu wanafunzi wenzao. Hakuna atakayetii mkubwa au mdogo mwenzake. Wanaonelea kiboko ni kama hakimu kwa wanyonge shuleni.

Wanashikilia uzi huo huo kwa kusema baadhi ya wanafunzi waliweza kuwa nadhifu tu kwa sababu ya adhabu ya viboko hasa ilichukuliwa kuwa baadhi ya wanafunzi wavulana wasingeweza kuoga hata kwa mwaka mzima labda siku ya krismasi tu iwapo kiboko kisingetumiwa. Hivyo kiboko kiliwasaidia kustawisha afya yao.

Mkondo huu wa hapo awali umeendelea kupingwa na wanamapinduzi ambao kwa nguvu zao zote wamesema utumiaji wa kiboko kama njia ya kustawisha nidhamu ni kukiuka haki za kibinadamu hasa zile haki za watoto ambazo zinastahili kulindwa na watu wote. Si walimu ambazo zinastahili kulindwa na watu wote. Si walimu si wazazi na si jamii kwa ujumla.

Nakumbuka kisa kimoja nikiwa shule ya msingi miaka ya 1980 ambapo kulikuwa na mwalimu mmoja aliyeitwa simione. Alikuwa amefangua kituo alichokiita “police station” katika eneo la shule ambacho kilitengewa waliokosa shuleni. Mwalimu huyu angeweza kufika shuleni saa tisa wakati wa majogoo ambapo tukikuwa tunashindwa iwapo alikuwa akilala kwake kulipokuwa takriban kilomita ishirini na tano au pale shuleni. Kila mwanafunzi aliyerauka afika shuleni kabla yake alijikuta ameingizwa kwenye hiki kituo cha polisi ambako angepingwa mijeledi kwelikweli.

Hali hii iliathiri wanafunzi wengi na hakuna aliyeweza kuwatetea. Baadhi yao waliweza kujeruhiwa vibaya wengine wakalazwa hata hospital. Wengine walioshindwa kufika shuleni kwa sababu ya umbali waliotoka waliweza kukosa shule. Kwa vile walihofia

kupingwa. Isitoshe, wengine waliofika kuchelewa waliweza kujificha manyasini na kuangalia kilichoendelea shuleni kwa umbali kasha walingojea tu adhabu ilipoisha na mwalimu simeone kuondoka upeoni mwa macho yao waliweza kutimka mbio kutoka mafichoni mwao wakiviziavizia hadi wakaingia darasani.

Hasara zilikuwa nyingi sana kwa wanafunzi kwa sababu baadhi ya wanafunzi walikiga kugumishwa kutokana na micharazo ya mara kwa mara hivyo wakawa wamezoea kupigwa pasi kuhisi uchungu wowote ikatokea kuwa walikuwa sasa watundu waliopita kiasi. Baadhi yao wakawa sasa na mtazamo mbaya kumhusu mwalimu simione.

Kwa kweli kilicho na mwanzo huwa kina mwisho wake. Ilitokea asubuhi moja mwanafunzi mmoja wa darasa la saba aliyeitwa opili alichelewa kumpiku mwalimu Simione kufika shuleni. Alipofika tu mwalimu akamuamuru, “Police Station mara moja” naye Opili akasita na kujifanya kutosikia.
Mwalimu akarudi yale yale naye Opili akawa hatendi alivyoamviwa. Mwalimu alipandwa na ghadhabu akamcharaza Opili kibao kimoja mara akadondoke chini na kuzimazi! Walijaribu kumpa huduma ya kwanza lakini wapi! Ilichukua juhudi kubwa sana baada ya kupata msaada kutoka hospitali ndipo hali ya kawaida ikarejea. Kutokea siku hiyo mwalimu simione alikorna shughuli hizo na akaomba msamaha wahusika wote.

Ndio sababu siku hizi kuna njia mbadala zinazoweza kutumiwa kukabiliana na ukosefu wa nidhamu kama vile kutumia njia ya ushauri na uelekezi, vilevile tunaweza kufunza motto mkorofi uzuri na ubaya wa vitendo anavyoshiriki, isitoshe tunaweza kutumia wanafunzi wenzake kushauri mhusika au kutumia watawala wa shule. Wakati mwengine kulifahamu tatizo linalomhusu mwanafunzi na chanzo chake huenda likasaidia sana kustawisha nidhamu na ikiwezekana kushirikisha wazazi wake.

MASWALI

a. Ipe taarifa hii anwani mwafaka (Alama 1)

b. Vitaje vikundi viwili ambavyo vimezuka kuhusu matumizi ya kiboko kama njia ya kulinda nidhamu kwa mijibu wa taarifa hii (Alama 1).

c. Wanaong'ang'ania kudumishwa kwa adhabu ya kiboko shuleni wanadai ina manufaa gain? (Alama 4).

d. Zitaje sifa zozote hasi mbili za mwalimu simione wa kifungu hiki (Alama 2).

e. Wanafunzi wa kifungu hiki waliathirika vipi na hatua za mwalimu Simeone? (Alama 4)

f. Taja njia zozote tatu zinazoweza kutumiwa badala ya kiboko kuweza kustawisha nidhamu shuleni kwa mujibu wa hadithi hii (Alama 3).

g. Taja mfano wowote mmoja mmoja uliotumiwa katika kifungu hiki kwa kila mbinu ya lugha ifuatayo: (Alama 2)

(i). Methali

(ii). Chuku

h. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu hiki: (Alama 3)

(i). Shinikizo

(ii). Kugumishwa

(iii) Kumpiku

SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (Alama 50)

3. a). Andika katika wingi: (Alama 1)
chuma cha kujengea choo kimepelekwa katika chuo kile.

b. Geuza sentensi hii iwe katika wakati ijao hali hali ya kuendelea (Alama 1).
Nilikuwa nikisoma alipofika nyumbani

c. Sahihisha: (Alama 2)

“ Haustahili kuyaleta madawa ya kulevya shuleni”, Juma alimweleza.

d. Ni ala zipi zinazotumiwa kutamkia vipasuo vifuatavyo?
Andika mfano mmoja mmoja wa neon kutofautisha maana. (Alama 2)
/P/ na /b/

e. Badilisha sentensi hii iwe katika kauli ya kutendwa (Alama 1)
Mkuvugenzi yule alikata simu yangu.

f. Andika aina mbili za vitenzi vilivyotumika katika sentensi ifuatayo kasha uonyeshe mfano kwa kila aina: (Alama 2)
Mgonjwa yule alitaka kufa akatibiwa.

g. Akifisha
Ah sikutarajia Naomi afike hapa Naivasha (Alama 3).

h. Kwa kuzingatia mfano wa kwanza uliopewa tumia maneno yanayofuata kukamilisha sentensi. (Alama 3).
Mfano: Punda wale kumi na wawili warefu weusi wameanguka.
Mikoba_____
Nazi _____

i. Tofautisha maana kati ya sentensi hizi: (Alama 2)
Wanafunzi walimchekea mwalimu
Wanafunzi walimchekelea mwalimu

j. Ainisha sentensi hii (Alama 2)
Aliyenisemeza

k. Andika katika usemi halisi: (Alama 3)
Asha alimwuliza dadake kiasi cha pesa ambazo angehitaji kwa matumizi ya shuleni.

l. Tumia vielelezo tungo kuchanganua sentensi ifuatayo (Alama 5)
Mkulima aliukata mti

m. Sentensi ifuatayo ni ya aina gan? Toa sababu mbili ya jibu lako (Alama 3)
Mwalimu mgeni amefika darasani mapema leo asubuhi na amefundisha somo la Kiswahili vizuri sana.

4. a. Ni methali ipi yenye maana sawa na ifuatayo (Alama 1)
Zimwi likujualo halikuli likakuisha.

b. Andika jozi mbili za vitate vilivyotumiwa katika sentensi ifuatayo kasha utofautisha maana ya kila neon. (Alama 4).

Bibi mwenye pipi zile alipakwa upupu na bubu yule.

c. Tegua kitendawili kifuatacho: (Alama 1)
Samaki wangu aelea kimgongomgongo

d. Pingu zinazotumiwa na polisi kuwanasia wahalifu pia huitwa
_____ (Alama 1)

e. Kabla ya mshukiwa kupelekwa mahakamani huwekwa _____ kasha akishahukumiwa huwekwa _____ (Alama 2)

f. Chuo chenu kiko chini ya wizara gain nchini kenya?_____(Alama 1)

g. Eleza maana ya semi ziguatazo (Alama 2)

i). Kazi ya kijungu jiko:_____

ii). Nguo kurudi:_____

h. Tunasema: Alikula chakula akamaliza fiju! Kisha alipoenda nyumbani kwao alizama_____ (Alama 1)
i. Tunga sentensi tatu tofauti kudhihirisha maana tofauti za neon zima (Alama 3)
j. Sayari ya tatu kutoka lilipo jua huitwa _____ (Alama 1)
k. Katika Hesabu umbo linalofanana na mwezi mchanga unapoonekana angani huitwa _____ (Alama 1)
l. Ugonjwa unaosababisha vidole vya miguu hata mikono kukatika huitwa _____ (Alama 1)

m. Mwenyeji anayekimbilia usalama katika nchi yaki mwenyewe huitwa _____ (Alama 1)

SEHEMU YA NNE: SAJILI (ALAMA 10)

5. Soma mazungumzo yafuatayo kasha ujibu maswali

Mtu I: Karibuni wateja karibuni viti
Mtu II: (Akiingia na mwenzake wanakaa)
Asante.
Mtu I: (Akiwaendea)
Yes customer tuwasaidiaje?
MtuII: Niletee menyukwanza
(Analetewa kasha anaangalia na kusema)
Mie ngo'mbe. Sorry nyama choma full kwa
Sembe kasha huyu mwenzangu utamletea chips kwa kuku karanga half.
Mtu I: Hivyo tu au mtahitaji zaidi?
Mtu II: Hee! Ndio, tutahitaji soda. Au vipi mwenzangu?
Mtu III: Darling me, I'll take pineapple juice
Mtu II: Ok! Sawa. Mletee hiyo sharubati ya nanasi nami uniletee Fanta baridi.
Mtu I: Jisikieni huru tafadhali. Nawaletea hivi punde (Akiondoka)

MASWALI

a. Hii ni sajili gain?_____ (Alama 1)

b. Eleza muktadha wa mazungumzo haya (Alama 2)

c. Andika na kuthibitisha sifa za sajili hii kwa majibu wa dondoo hili (Alama 5)

d. Ni sifa zipi za sajili hii ambazo hazijitokezi katika kifungu hiki? (Alama 2)

<u>MWONGOZO</u>

2. Ufahamu

a. Nidhamu/ matumizi ya kiboko / kiboko

(yoyote 1 x 1= 1)

b. Wanamapokeo (Alama ½ x 1= ½)

Wanamapinduzi (Alama ½ x 1 = ½)

c. Manufaa:

- Wanafunzi kutia bidii masomoni
- Hustawisha nidhamu
- Kazi kutekelezwa kwa urahisi
- Kuwezesha utaratibu wa shule kufuatwa
- Wanafunzi wanafika shule mapema
- Wataingia darasani mapema
- Wataheshimu wanafunzi wenzao
- Wanafunzi kuwa nadhifu

(Pointi zozote 4 x Alama 1= 4)

d. Sifa hasi za simeone

- Katili kwa kuiga wanafunzi
- Mwenye hasira kwa kukasirishwa na mwanafunzi Opili

(Zozote 2 x 1 = 2)

e. Wanafunzi walivyoathirika

- Kupelekwa “police station” na kupigwa.
- Kutishika wakihofia mwalimu Simeone
- Kujificha kutoka mwalimu Simeone
- Baadhi yao waligumishwa na kutojali adhabu wakawa watundu
- Baadhi waliacha na kukosa kuja shule.
- Opili alizimia zi!

(Zozote 4 x 1 = 4)

f. Suluhisho badala ya kiboko:

- Njia ya ushauri na uelekezi
- Kueleza watoto wakorofi ubaya wa ukorofi na uzuri wa nidhamu
- Kutumia ushauri wa wanafunzi wenzao
- Kushirikisha utawala wa shule
- Kulifahamu tatizo la mwanafunzi na chanzo chake
- Kushirikisha wazazi wa mwanafunzi

(Zozote 3 x 1 = 3)

g. (i). Methali

- Kilicho na mwanzo hakikosi mwisho
- Kila mwamba ngoma ngozi huvutia kwake.

(Yoyote 1 x 1 = 1)

(ii). Chuku

- Wavulana kukosa kuoga hata mwaka mzima labda siku ya krismasi
- Mwalimu Simione kufika shule saa tisa kable mwanafunzi yeyote kuingia kutoka umbali wa kilomita 25.
- Wanafunzi kugumishwa na kupigwa wakawa hawahisi uchungu

(yeyote 1 x 1 = 1)

h. (i) Shirukizo – Msukumo / kulazimishwa

(Yoyote 1 x 1 =1)

(ii) Kugumishwa – Kufanywa kuzoea / kutosikia uchungu / kutojali

(Yeyote 1 x 1 = 1)

(iii) Kumpiku – Kumshinda

(1 x 1 = 1)

Adhibu jumla ya makosa

3 tahajia x ½ = 1 ½

3 sarufi x ½ = 1 ½

Usiadhibu zaidi ya nusu ya alama alizopata kwa kila swali.

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)

3. a). Vyuma vya kujengea vyoo vimepelekwa katika vyuo vile

(lazima apate zote ndipo apewe alama 1)

b). Nitakuwa nikisoma atakapofika nyumbani

(Lazima apate zote ndipo apewe alama 1)

c). "Hustahili kuzileta dawa za kulevya shuleni, Juma alimweleza

(Lazima apate zote ili apewe alama 2)

d). Ala zinazotumiwa ni:

mdomo wa juu (½ alama)

mdomo wa chini (1/2 alama)

mfano wa neon:

/p/ - papa (mfano wowote unaofaa ½ Alama)

/b/- baba (mfano wowote unaofaa ½ Alama)

e). Simu yangu ilikatwa na mkurugenzi yule (Alama 1)

f). Alitaka – kitenzi kisaidizi

kufa – kitenzi kikuu

Alitaka kufa – vitenzi sambamba

(Zozote 2 x 1 = alama 2)

g). Ah! Sikutarajia Naomi afike hapa. Naivasha.

(Zozote 6 x ½ = alama 3).

h). Mikoba ile kumi na miwili mirefu mieusi imeanguka

(Lazima pate zote ili apewe alama 1 ½)

Nazi zile kumi na mbili ndefu nyeusi zimeanguka

(Lazima apate zote ilie apewe alama 1 ½)

i). Walimchekea – walimfurahia (Alama 1)

Walimchekelea – walimfanyia mzaha / walimdharau (Alama 1)

j). Aliyenisemeza

A- Kiwakilishi cha nafsi ya tatu katika umoja

Li- Kiwakilishi cha wakati uliopita

Ni- Kiwakilishi cha mtendewa katika umoja

Sem – Shina la kitenzi

Ez – kiendelezi

a. Kimalizio


(Zozote 4 x ½ = alama 2)

k. "Dada! Unahitaji pesa ngapi kwa matumizi ya shuleni?" Asha aliuliza

- "Dadangu unahitaji pesa ngapi za matumizi ya shuleni?" Asha aliuliza
- "Unahitaji pesa ngapi za matumizi ya shuleni?" Asha aliuliza dadake

(Yoyote moja iliyozingatia uakifishaji 6 mwafaka x ½ alama 3)

l.



(al.1)

(½ al. + ½ al. = al.1)

(½ al + ½ al. + ½ al/ = 1 ½)

Mkulima Aliukata Mti (½ al. + ½ al. + ½ al. = 1 ½)

m. Sentensi ambatano (Alama 1)

- Ina vishazi huru viwili (sentensi huru mbili) (Alama 1).
- Imetumia kiunganishi “na” (Alama 1)

4 a). Damu ni nzito kuliko maji (Alama 1)

b). Bibi – Jina la heshima la kuita mwanamke / Nyanya (Alama 1)

Pipi – Peremende (Alama 1)

Bubu – Mtu asiyeweza kunena (Alama 1)

Upupu – Aina yam mea unaowasha mwili sana (Alama 1)

c). Merikebu (Alama 1)

d). Vikuku (Alama 1)

e). Rumande/ korokoro (Alama 1)

Jela (Alama 1)

f). Wizara ya Elimu (Alama 1).

g). i. Kazi ya kujipatia mahitaji ya chakula tu (Alama 1)

ii. Nguo kuwa fupi (Alama 1)

h). Alizama zi! (Alama 1)

i). Kikosi cha fanya fujo uone <u>kilizima</u> maasi ya wanafunzi

Baada ya moto kuenea sehemu ile uliweza <u>kuzimwa</u> na wataalamu hao.

Lile jitu zima linatenda mambo ya kitoto.

Nilipomwona alikuwa <u>mzima</u> bila tatizo lolote la kiafya

(Zozote 3 x 1 = 3)

j). Dunia (Alama 1)

k). Tao (Alama 1)

m). Mkimbizi wa ndani kwa ndani (Alama 1)

SEHEMU YA NNE: SAJILI (Alama 10).

5. a). Biashara ya hotelini (Alama 1)

b). Mazungumzo ni kati ya mhudumu wa hoteli na wateja.

Wahali ni hotelini

Wateja wanaitisha chakula na vinywaji

Mhudumu anaenda kuwaletea

(Zozote 2 x 1 = alama 2)

c). Upole / ukarima – Karibuni wateja. Karibuni viti

Jisikieni huru tafadhali

Matumizi ya msamiati wa hoteli – Mengu, soda, chips, sharubati, sembe, fanta Baridi , mle ngombe.

Utohozi – menyu

Lugha mseto – “Yes customer” sorry full, half, pineapple juice na kadhalika.

Urudiaji/ ukariri / Takriri – karibuni wateja. Karibuni viti

Udadisi – hivyo to au mtahitaji zaidi?

(Zozote 5 x 1 = alama 5)

d). Porojo na ujanja

chuku

(Zozote 2 x 1 = alama 2)